Baadhi Ya Majina Ya Ibilisi
(Some Of The Names For The Devil)

Na

Alex S. Silvester

Baadhi Ya Majina Ya Ibilisi

na

Alex S. Silvester

Novemba 16, 2017

Baadhi Ya Majina Ya Ibilisi

Kila mmoja wetu duniani ana jina ambayo tumepewa na wazazi wetu tulipozaliwa. Lakini zaidi sana tuna majina mazuri ambazo hazijawahi kuwepo duniani na majina hayo ni Wakristo ikimanisha sisi ni wake Kristo aliyeshinda mauti na sasa yuko katika mkono wa kuume wa Baba yake. Hataivyo, tusisahau kwamba majina yanamanisha kitu na kila kitu kina jina lake.

Ningependa tuangalie majina ambayo Shetani huitwa; biblia inataja baadhi ya majina ambayo Shetani huitwa na tunakwendaa kuangalia majina ishirini na saba kati ya hizo. Na kila jina linaelezea uwezo wake na ubinafsi. Kwa mtu kukataa kwamba Shetani hayupo; ili awe mkweli anapaswa pia kukataa uwepo wa Mungu, maana Biblia inatueleza vyote hivyo.

- **Mwovu,** "*Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja **yule mwovu**, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia.*" (Mat. 13:19). Bwana wetu alijua kwamba sio kila mtu atasikia neno lake na kulishika kwa sababu Shetani pia huzunguka na kutafuta roho zisizo imara.

- **Adui,** "*Yule adui aliyepambana na ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia, na wale wavunao ni malaika.*" (Mat. 13:39). Biblia inatuonya kuwa makini na werevu katika neno lake kama tusipokaa katika neno lake Shetani atatupeleka katika ufalme wake. Tukumbuke pia kwamba Shetani hatafuti wale walioko nje ya Kristo bali anatutafuta sisi tulio ndani ya Kristo.

- **Beelzebabu,** "*Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalemu wakasema, Ana **Beelzebuli**, na kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo.*" (Marko 3:22). Shetani anawaweka watu kwenye maumivu, ilitokea Yesu alipoingia kwenye sinagogi naa kumpata mtu alaiyepooza mkono.

- **Mkuu wa ibilisi,** "*…na kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo. Akawaita akawaambia kwa mifano, awezaje Shetani kumtoa Shetani?*" (Marko 3:22-23).

- **Mwenye nguvu,** "*Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha zake, alindapo nyumba yake vitu vyake vi salama.*" (Luka 11:21)

- **Muuaji, mwongo, baba wa uongo:** "*Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda, yeye alikuwa*

mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa huo." (Yohana 8:44). Anatudanganya ili tufanye anachotaka tufanye na sio anachotaka Mungu tufanye. Tunapaswa kuwa makini kwa sababu anazunguka kama simba angurumaye ili awape wadhaifu wa imani ili awaangamize.

- **Mkuu wa ulimwengu,** "*Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavu wote kwangu.*" (Yoh. 12:31-32).

- Shetani, "*Petro akasema Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja?*" (Mdo. 5:3). Tunapojaribiwa inatupelekea mauti. Tunasoma kuhusu wanandoa wawili waliouza sehem ya kiwanja na badala ya kupeleka fedha ile miguuni pa mitume, walificha sehemu ya fedha ile. Sababu iliyowapelekea kufanya hivyo ni kwamba Shetani aliwaingia na kuwadanganya na kuwasababishia kifo.

- Mungu wa ulimwengu huu, "*Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha vikra zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.*" (2 Kor. 4:4). Wakati injili ya Kristo inahubiriwa wengine wanasinzia au wanafikiria kuhusu mambo mengine ambazo hazipo katika mambo wanayosikia au kufanya. Lakini napenda sehemu hii; **injili ya utukufu wake Kristo** ni jukumu letu kuwaambia kuhusu injili ili kwamba wawe huru kutoka katika mitego ya Shetani.

- Beliari, "*Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na **Beliari**? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini?*" (2 Kor. 6:15).

- Nyoka, "*Laiti mngechukuliana nami katika upumbavu wangu kidogo, naam, mchukuliane nani. Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi. Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo.*" (2 Kor. 11:1-3)

- Mkuu wa mamlaka wa anga, "*Ambapo katika wakati uliopita mlitembea kulingana na mwendo wa ulimwengu huu, kulingana na **mkuu wa mamlaka wa anga**, roho ambayo sasa inatenda kazi katika watoto wa kutotii:*" (Efe. 2:2).

- **Mjaribu,** "*Kwa hiyo mimi nami nilipokuwa siwezi kuvumilia tena, nalituma mtu ili niijue imani yenu, asije yule mjaribu akawajaribu, na taabu yetu ikawa haina faida.*" (1 Thes. 3:5).

- Mshitaki, "*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi kama simba angurumaye, huzunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze.*" (1 Pet. 5:8). Tunaonywa kuwa makini tusije tukaanguka katika mitego ya shetani nah ii itatokea tu tukikaa katika neno lake. Tunaposoma na kujifunza.

- Malaika wa kuzimu, "*Na juu yao wanaye mfalme, naye ni malaika wa kuzimu, jina lake kwa Kiebrania ni **Abadoni**, na kwa Kiyunani ni analo jina lake **Apolioni**.*" (Ufu. 9:11). Kuna majina mawili tofauti katika majina mawili tofauti ya Biblia na hii ni **Kiyunani** (Apolioni) na **Kiebrania** (Abadoni).

- Joka kubwa jekundu, joka, joka mkubwa, nyoka wa zamani, ibilisi, shetani, mwongo wa ulimwengu huu, mshitaki, "*Ikaonekana ishara nyingine mbinguni na tazama **joka mkubwa jekundu**, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba…*" (Ufu. 12:3-10). Tunapaswa kuwa makini kwa kila kitu ili kwamba tuwe mbali naye (Shetani). Wengi tunaanguka kwa sababu anakuja na mvuto na uzuri wa maneno ili kwamba tumkubali. Tuna weza kumwepuka kwa kusoma na kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

Mungu wetu na atusaidie kumshinda mwovu tunapoendelea kumtumikia katika shamba lake.